# Je Wataka Kuwa Mzima?

**na**

**Ellis Forsman**

# Je Wataka Kuwa Mzima?

**na**

**Ellis Forsman**

**Januari 17, 2012**

# Je Wataka Kuwa Mzima?

## Yohana 5:1-16

Yohana 5:6, "*Yesu alipomwona huy amelala, naye akijua ya kuwa amekuwa hali hiyo siku nyingi, alimwambia wataka kuwa mzima?*"

Watu hawana ukamilifu kwamba wanataka kuji bidiisha ili waponywe. Hakuna mtu aliye mkamilifu, lakini tunatakiwa tujibidiishe ili tuufikie ukamilifu. Kama tunavyoona mtiririko katika maisha yetu, tunafanya kila tuwezalo ili kuweza kutibu tatizo na kuwa safi sisi wenyewe.

Tuna sehemu nyingi katika miili yetu ambazo zinaufanya mwili kukamilika, na kila kiungo kipo katika hali ya kutokamilika ambayo inahitajika kuweza kutibiwa.

Mwanadamu anamwili wa nyama. Ana nyama, damu, viungo vya kuhisi, mifupa, nk. Mwili unakula, unalala, unatembea, unaongea, sehemu tano za kuhisi zinafanya kazi, na kufanya vitu vingi vya kazi ya kimwili.

Mwanadamu ana upeo. Huo ni, uwezo wa kiakili. Anaakili. Upeo wa juu unaozingatia, kufikiria, unatengeneza hitimisho, unakubali, unaamini, unakataa, unaamini.

Mwanadamu anahisia. Anahisia zinazo chukia, penda, furahia, omboleza, nk.

Mwanadamu ana mapendekezo. Mapendekezo hayo yanachagua, na kuamua.

Mwanadamu anadhamira. Dhamira inathibitisha tunapofanya kitu tunachofikiria kuwa ni sahihi, na kuhukumu pale tunapofikiria tumefanya kitu ambacho ni makosa.

Tunaweza kuelimishwa ili kutambua jema na baya, lakini matendo yake si ya kujitolea. Haitambui jema na baya, bali tu inathibitisha au kuhukumu.

## Sote tu wagonywa

Ni wangapi watu ambao ni wazima uliokwisha kuwaona? Si ni jambo la kushukuru kuwa mzima?

### Hakuna miili ambayo ni mikamilifu.

Kimwili, miili yetu inapata baridi na maradhi mengine, tunatoa damu tunapojikata, mifupa yetu huvunjika, nk.

Wengine wana kumbana na majanga tofauti; na wengine wazaliwa hivyo.

Kuna miili mirefu ambayo ni mirefu na inapatashida kuingia katika vyumba, au kulala sehemu fupi; kuna miili ambayo ni mifupi na inapatashida kucheza mchezo wa pete, au kufikia kinyagio cha mafuta cha gari.

Kila mtu anawazo lake mwenyewe ya jinsi ambavyo mwili iliyokamilika unavyopaswa kuwa. Kiasi au muundo wa mwili wa mtu haihusiani na utakatifu wa mwili huo.

## Kwa ukamilifu hakuna akili ambazo ni sawa.

Sisi sote kwa kiwango fulani ni wehu.

Kuna wengine wana akili za kufikiria na wengine akili za hisia. Hizi akili tofauti wakati mwingine zinapata wakati mgumu wa kuelewana sisi kwa sisi.

Kila aina ya akili ina kazi yake, na kila moja inatabia yake katika kujirudi nyuma.

Akili inayofikiria zaidi huwa tayari kusoma na kukubali neno la Mungu, lakini inaweza kuwa na shida kuelewa hisia za wengine. Mara nyingi haipendi matakwa ya hisia juu ya mantiki.

Akili ya hisia hufanya vizuri katika kuwa kubali watu na mahitaji yao, lakini inaweza kuwa na shida katika kukubali neno la Mungu kama amri. Maranyingi haipendi hisia za kimantiki, na inaweza kujifanya kuwa kimya na kupata dharura. Mara nyingi haichunguzi mambo, bali hufanya kazi kama ilivyo.

Kila aina ya akili ni muhimu, lakini kila mmoja lazima ielewe udhaifu wake. Kuna tabia ya mtiririko wa akili.

Kuwa wamilifu lazima tuelewe haya mambo tofauti za ubinadamu na kufanya kila tuwezalo ili kuweza kushinda makosa yetu.

Kila mtu lazima ajifunze msimamo wa utu wetu. Hatuwezi kuwa safi kama kama tunafanya mambo pasipo hisia yo yote, au ishara yoyote ya kuweza kuepuka ukweli wowote.

## Watu wanatofautiana katika dhamira zao.

Yeshwa kwamba wanatakiwa wafanye kitu juu ya swal hil

Zaidi sana baadhi ya dhamira za watu zimechomwa kiasi kwamba zinafikia kiwango hazijali. Hii ni dhamira inayoumwa, na si safi.

Dhamira za watu wengine hazija fundishwa vizuri, hazijawekwa katika msingi wa neno la Mungu.

# Je Wataka Kuwa Mzima?

Badala ya kujiachia sisi wenyewe katika mapenzi yetu, tunahitajika tumruhusu Yesu Kristo aongoze uwepo wetu wote bila kitu kingine kiongoze, litawale na kutushinda.

## Miili yetu.

Wengine wanapoonyeshwa udhaifu wao, na kuonyeshwa kwamba wanaweza kufanya kitu juu ya yake, wanakuwa wagumu na kusema kitu kama, "Ni maisha yangu", au "Ni mwili wangu". Kuna vitu vya kudhuru vinavyoweza kufanywa katika mwili na kuufanya usiwe safi.

"Ni maisha yangu", "Ni mwili wangu, wanasema. Je ndivyo ilivyo?

Tuna miili ya mapendekezo; hiyo ni, tuna matakwa ya kufanya uchaguzi. Tunaweza kuchagua.

- 1 Wakor. 6:19-20, "*Au hamjui yakuwa mwili wenu ni hakalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mli nunuliwa kwa thamani. Sasa basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu."*
- 1 Wakor. 3:17, "*Kwa sababu hii nimemtuma Timotheo kwenu aliye mwanangu mpendwa, mwaminifu katika Bwana, atakayewakumbusha njia zangu zilizo katika Kristo, kama vile nilifundishavyo kila mahali katika kila Kanisa.*"

## Akili zetu.

Wale walio na akili za kufikiria wanaiharibu kama ikiwa kile wanachokipata cha ujuzi na takwimu wanaacha neno la Mungu.

- Wafil.3:7-8, "*Injili hiyo ambayo nalifanywa mhudumu wake, kwa kadiri ya kipawa cha neema ya Mungu niliyopewa kwa kadiri ya utendaji wa uweza wake. Mimi niliyemdogo kuliko yeye aliye mdogo wa watakatifu wote, nalipewa neema hii ya kuwa hubiri Mataifa utajiri wake Kristo usiopimika.*"
- 2 Wakor. 10:5, "*Tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu, na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo.*"

Kuwa na akili safi ni kuwa na akili inayopenda kujua mapenzi ya Mungu, na kutupilia mbali fikira na mawazo ambayo yako kinyume na mapenzi yake.

## Hisia zetu.

Hisia inaweza kuwa kitu chenye nguvu katika maisha yetu; lakini tunapaswa kuchukua kinga ili ili hisia zetu ziwe safi.

Vita vingi na damu nyingi zisizohitajika zimesababishwa kwa sababu ya hisia za mtu Fulani zenye chuki., au kutaka kupata na kingine.

Familia zimevunjika kwa sababu ya hisia za mtu Fulani zenye nguvu kwa mtu Fulani kuliko mwenza wake mwenyewe.

Hisia za chuki, upendo, furaha, na maombolezo ni nzuri na sahihi katika mtazamo sahihi.

- Hatupaswi kuwachukia ndugu zetu, bali tuchukie dhambi.
- Tunapaswa kupendana sisi kwa sisi, lakini bila upendeleo.
- Tunapaaswa kuwapenda wake zetu kiukweli, lakini upendo wetu wa kindugu unapaswa kuwa wa kindugu.
- Tunapaswa kufurahi na hao wanaofurahi, na kulia na hao waliao. Kufanya kinyume hatutakuwa safi kihisia.

Watu wengine wanaingiwa na shauku, wakati wengine wanakoswa. Waati ambapo mengi mazuri yanaweza kufanywa na mtu mwenye wingi wa shauku; uharibifu mwingi unaweza kufanywa kama haija pangiliwa na neno la Mungu.

Waru. 10:1-2, "*Ndugu zangu nitakayo sana moyoni mwangu na dua yangu nimwombayo Mungu ni kwa ajili yao ili waokolewe. Kwa maana nawashuhudia kwamba wanajuhudi kwa ajili ya Mungu, lakini si katika maarifa.*"

Kuna dhamira nyingi ambazo ni nzuri, watu wenye shauku mbaya wanaongoza watu wengi katika upotevu wa uziam kwa sababu ya kujali kwao kudogo katika neno la Mungu, wakichezea hisia za watu wengine.

## Matakwa yetu.

Mwanadamu ana mwili wenye maamuzi, hiyo ni, ana matakwa ya kufanya mambo.

Kulikuwa na msemo uliozoeleka katika miaka ya 1980, "Naweza kufanya kile ninachotaka kukifanya; na kuwa kile ninachotaka kuwa; na kusema kile ninachotaka kusema." Aina hii ya matakwa ni kinyume na matakwa ambayo Mungu anataka tuwe nayo.

- Yohan 7:17, "*Mtu akipenda kuyatenda mapenzi yake atajua habari yay ale mafunzo, kwamba yatoka kwa Mungu au kwamba mimi nanena kwa nafsi yang utu.*"

- Math.5:6, "*Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa.*"

Matakwa iliyo sahihi inaonyesha nia ya kutafuta haki ya Mungu na kumruhusu aongoze maisha yetu.

## Dhamira yetu.

Kwa kuwa dhamira ni uthibitisho wa haki au kutokuwa kithibitisho cha mabaya, inaweza kuwa muongozo mzuri cha kuangalia kama tuna miili safi au akili?

**Siyo na Paulo.**

- Matendo. 26:9-12, "*Kweli mimi mwenyewe naliona ndani ya nafsi yangu kwamba yanipasa kutenda mambo mengi yaliyopingamana na jina lake Yesu Mnazareti; nami nikayafanya hayo Yerusalemu; niliwafunga wengi miongoni mwa watakatifu ndani ya magereza, nikiisha kupewa amri na wakuu wa makuhani; na walipouawa nalitoa idhini yangu. Na mara nyingi katika masinagogi yote naliwaadhibu, nikawashurutisha kukufuru, nikawaonea hasira kama mwenye wazimu nikawaudhi hata katika miji ya ugenini. Basi katika kazi hiyo nilipokuwa nikienda Dameski, mwenye mamlaka na maagizo ya wakuu wa makuhani.*"

- 1 Tim.1:5, "*Nikiikumbuka imani uliyo nayo isiyo na unafiki ambayo ilikaa kwanza katika bibi yako Loisi, na katika mama yako Eunike, name nasadiki wewe naye unayo.*"

# Kusudi halisi la Yesu kuja

Kwamba wanadamu lazima wafanywe wazima.

- Yohana 10:10, "*Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu, mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele.*"

- 2 Tim.3:15-17, "*Na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu iliyo kwa imani ya Kristo Yesu. Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"

Lazima wafanywe safi kupitia maandiko.

2 Wakor. 3:18, "*Lakini sisi sote kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na*

*mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.*"

# Hitimisho

Je wewe ni safi?

Je wewe ni mgonjwa au dhaifu kiroho?

Kama wewe si safi, kwa nini usimruhusu Yesu akuponye kupitia kukubali kwako na kumtii yeye.

Kuwa safi mtu anatakiwa kuwa Mkristo. Yafuatayo ni hatua muhimu za kufanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb.11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*" nilipokuwa katika shule ya sekondari (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na wa kwangu alikuwa hamuamini Mungu. Kwa vile nilikuwa nimebatizwa, nilichukua nafasi kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kuwa kuishi maisha ya Ukristo ni nzuri, lakini hakuamini kwamba alimwamini Mungu. Lakini ili awe upande sahihi, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbelel za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba amekwenda kanisani na kuishi maisha mazuri kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyiki hivyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza."

- **Toba.** Matendo. 2:38, "*Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Matendo 11:18, "*Waliposikia maneno haya wakanyamaza, wakamtukuza Mungu wakisema, Basi, Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima*". Ikiwa ulikuwa umelala , ukasikia sauti kutoka katika chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "kuna mwizi katika nyumba yangu!" hivyo unachukua simu ya mkononi, taratibu uwezavyo, unawaita polisi, ukiwaambia kuna mwizi katika nyumba yako, na unawapa anuani ya nyumbani kwako. Kidogo, wanafika na kumshika mwizi. Anapiga kelele, "Samahani; Samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na si kwamba ameiba na anataka kubadilisha maisha yake. Katika toba ya kweli. Ni badiliko la akili

(nia) inayoleteleza badiliko la tendo. Hicho ndio tunatakiwa kufanya kabla hatuja fanyika Wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata wokovu na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*" tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

  Zingatia kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamaanisha kuelekea kitu fulani; si kwamba mtu tayari ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ambapo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe alibatizwa kutimiza haki yote, " ". (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi kufanya. Je unaona jinsi Mungu alivyopendezwa wakati Yesu alipobatizwa? Yesu pia anasema "*imekuwa **kwetu** kuitimiza haki yote.*" Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake, si kw sababu ni haki yetu.

  Kwa kweli, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapoke kipawa cha Rpho Mtakatifu.*" (Matendo 2:38). Petro, ulisema ni nini kusudi la ubatizo? "*kwa ajili ya ondoleo la dhambi".* Kwa nini mtu anataka kuacha au kuondoa hatua hii muhimu ya ubatizo unaotuondoa dhambi zetu?

  Yesu aliamuru kwamba ili kufikia wokovu ni lazima tubatizwe. "*Akawaambia, enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Marko16:15-160).

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Sasa unakawilia nini? Simama, ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, huku ukiliitia jina la Bwana.*" (Matendo 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu. " ." (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu kwa kupaka damu ya Kristo katika maisha yetu kwa kubatizwa. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

  Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatupeleki mwili makaburini na kuweka udongo kidogo juu yake; bali tunauzika.

Kama hujawa Mkristo, kwa nini usianze leo?